

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dodoma
21 Oktoba, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SERIKALI KUIMARISHA MAZINGIRA YA UCHIMBAJI MADINI - RAIS SAMIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewaasa wachimbaji wadogo kuachana na vitendo vya utoroshaji madini.

Rais Samia ametoa wito huo leo wakati akihutubia kwenye hafla ya uzinduzi wa mitambo ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo pamoja na mitambo ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Aidha, Rais Samia amesema wachimbaji wadogo hawana budi kuunga mkono jitihada za serikali kwa kuhakikisha kuwa wanauzu madini yao katika viwanda vya ndani vya kusafisha dhahabu ili kuchochea uchumi wa viwanda.

Vile vile Rais Samia amewataka wachimbaji hao kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika sekta ya madini ili kuhakikisha kuwa rasilimali za madini zinawanufaisha wananchi na kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi.

Rais Samia pia amewahakikishia wachimbaji wadogo wa madini nchini kwamba serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mazingira ya uchimbaji pamoja na biashara ya madini ili waweze kuchangia kwenye uchumi wa taifa.

Serikali ina mpango ambao ni sehemu ya Dira ya 2030 (*Vision 2030*) unaoelekeza kufanya utafiti wa madini kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya "*High Resolution Airborne Geophysical Survey*" ifikapo mwaka 2030.

Kama hatua za mwanzo za utekelezaji wa mpango huo, mitambo mitano yenye thamani ya shilingi bilioni 2.73 imezinduliwa ambayo iko tayari kufanya kazi katika maeneo ya wachimbaji wadogo hapa nchini.

A blue ink signature of Zuhura Yunus, the Secretary General of the Office of the President.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

